*Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 198-216*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i2.4

# Dhima za Umatinishaji-upya[1] katika Fasihi: Uchunguzi Kifani wa Nyimbo za Muziki wa Dansi na Ngano

*Angelus Mnenuka*[2]

**Ikisiri**

Kila jamii ina utamaduni ambao hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Njia mojawapo ya urithishaji wa utamaduni katika jamii inayobadilika ni umatinishaji-upya wa matini. Huu ni mchakato wa kuichopoa matini kutoka katika muktadha wake asilia na kuichopeka katika muktadha mpya. Nchini Tanzania, kumekuwa na utaratibu huu pia ambapo hotuba mbalimbali za Mwalimu Julius K. Nyerere hurushwa na kituo cha TBC Taifa kila siku katika kipindi kijulikanacho kama 'Wosia wa Baba'. Halikadhalika, nyimbo mbalimbali zilizopigwa miaka iliyopita huendelea kupigwa ili kurithisha tunu mbalimbali kwa kizazi cha sasa. Makala hii inajadili hotuba ya Mwalimu Nyerere iliyohusisha utambaji wa ngano. Ngano hii inahusu wanaume waliogeuka kuwa mawe baada ya kutetereka kimsimamo. Hotuba hii ilienea na kusambazwa mwanzoni mwa mwaka 2016 wakati Rais John P. Magufuli wa Tanzania alipokuwa akifichua uozo serikalini muda mfupi baada ya kuapishwa. Sambamba na hotuba hiyo, wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" ulioimbwa na bendi ya Asilia Jazz ulisambaa katika mitandaopepe ya kijamii. Katika makala hii, inaelezwa kuwa kusambaa kwa kipande hicho cha hotuba na wimbo huu, mahususi katika kipindi tajwa, ni sehemu ya umatinishaji-upya wa matini wenye lengo la kuibua kumbukumbu na kuwatia moyo viongozi katika vita dhidi ya ufisadi na kuleta matumaini mapya ya kutetea wanyonge.

## 1.0 Utangulizi

Katika maisha, binadamu hutumia matini za aina mbalimbali katika mawasiliano (Hanks, 1989; Bauman na Briggs, 1990; Barber, 2007). Matumizi ya matini kutoka vyanzo mbalimbali katika mawasiliano ya kawaida na yale ya kisanaa yalishaelezwa hapo awali na Mikhail Bakthin. Hata hivyo, maandiko yake hayakujulikana mapema katika maeneo mengine ya dunia, hususani nchi za Kimagharibi kwa sababu ya hali tete ya kisiasa wakati huo nchini Urusi na tofauti za mikabala ya uandishi wake na ule wa Kimagharibi (Holquist, 1981). Baadhi ya

---

[1] Istilahi hiyo ni tafsiri ya istilahi ya Kiingereza *entextualisation* iliyofafanuliwa na kutumiwa na Bauman na Briggs (1990), Urban (1996) na baadaye kutumiwa na wanazuoni mbalimbali.

[2] Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: amnenuka@gmail.com

wanazuoni wanadai kuwa mawazo ya Bakhtin yalianza kutolewa na mwanazuoni wa Kibulgaria aitwaye Julia Kristeva aliyesoma kazi za Bakthin (Alfaro, 1996; Pechey, 2007; Orr, 2011). Miongoni mwa dhana zinazotokana na mawazo ya mwanazuoni huyo wa Kirusi ni mwingilianomatini. Kifupi, mwingilianomatini kwa misingi iliyowekwa na maandiko ya Bakhtin ni matumizi ya dhana, kauli, maneno au mawazo yaliyotolewa na wengine. Kwa hakika, kila mtu anazungumza na kutumia misemo, dhana, mawazo, kauli, semi na mitindo iliyoanzishwa na wengine (Bakhtin na Holquist, 1981). Hata hivyo, binadamu haishii tu kutumia dhana, kauli, maneno au mawazo bali hutumia matini pana zaidi kwa kuzitoa katika muktadha mmoja na kuzitumia upya katika muktadha mwingine kwa malengo mbalimbali (Silverstein na Urban, 1996). Mchakato wa kuiondoa matini katika muktadha wake, yaani uziduaji, na kuipeleka katika muktadha mwingine unajulikana kama *umatinishaji-upya*[3] (taz. Bauman na Briggs, 1990; Silverstein na Urban, 1996; Urban, 1996). Kwa ujumla, umatinishaji-upya umefumbata vipengele vyote vya mwingilianomatini kwani haushii tu kutumia matini A katika matini B, bali matini iliyoziduliwa hutazamwa kama matini mpya katika muktadha mpya.

Tofauti kubwa baina ya mwingilianomatini na umatinishaji-upya ni kwamba mwingilianomatini ni utumiaji wa matini zilizotumiwa na watu wengine (Blommaert, 2005). Kwa maneno mengine, mwingilianomatini ni uhusiano wa matini moja na nyingine (Gross, 2001). Wakati huohuo, umatinishaji-upya ni mchakato wa kuizidua matini katika muktadha wake wa utendaji na kuichopeka katika muktadha mwingine wa utendaji ambapo inakuwa matini nyingine tofauti na ile ya awali (Blommaert, 2005). Kwa hiyo, umatinishaji-upya unaongeza sifa ya mwingilianomatini na kuifanya dhana hii kuwa kiunzi cha kiutafiti (Blommaert, 2005:47). Hivyo, umatinishaji-upya unaanzia pale mwingilianomatini unapoishia kwani msingi wa umatinishaji-upya ni matini pamoja na muktadha au kilongo.

Julius Kambarage Nyerere, anayejulikana pia kama Mwalimu Nyerere, alikuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika, baadaye Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (1962-1985). Aidha, Nyerere aliongoza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na kuwa mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine kwa uadilifu wake katika matumizi ya mali ya umma. Kama kiongozi mkuu wa kwanza wa nchi, katika miaka ya awali, alikabiliana na jukumu kubwa la kujenga mfumo wa jamii mpya katika nchi huru. Inaonekana haikuwa kazi rahisi kwake kuendeleza mfumo wa kikoloni ikizingatiwa kuwa mifumo ya kikoloni iliengua mila na tamaduni nzuri za Kiafrika (Nyerere, 1966). Kwa hiyo, Nyerere alitamani kurejesha tamaduni na tunu za Kiafrika zilizoondolewa na ukoloni. Changamoto hizo za namna ya kujenga jamii mpya katika nchi huru ziliwakabili viongozi wengine wa Kiafrika akiwamo Kwame Nkrumah, Rais wa Kwanza wa Ghana

[3] Ni kisawe cha neno la Kiingereza *entextualisation.*

ambapo, tofauti na Nyerere, yeye alipendelea kuwa na mseto wa tamaduni kwa manufaa ya ujenzi wa jamii mpya (taz. Nkrumah, 2009).

Baada ya kupata uhuru mwaka 1961, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi zilizofanya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi barani Afrika. Miongoni mwa mageuzi hayo ni kutangazwa na kutekelezwa kwa baadhi ya maazimio ya Azimio la Arusha 1967 (Ibhawoh na Dibua, 2003). Azimio la Arusha lilienda sambamba na ari ya kuondoa unyonyaji baina ya watu katika nchi huru. Kwa hiyo, hotuba mbalimbali za Mwalimu Nyerere zilizohamasisha kukata mirija ya unyonyaji zilienda sambamba na nia ya kuondoa tabaka la makabaila na mapebari uchwara. Kama ilivyo ada, baadhi ya kazi za sanaa zilizotungwa na kutolewa katika kipindi hiki ziliunga mkono msimamo wa serikali, yaani kudhihaki wanyonyaji na wakati huohuo kuwatia moyo viongozi kuendeleza mapambano ya kuimarisha Sera ya Ujamaa (Blommaert, 1999; Rettová, 2010; Mnenuka, 2019a).

Lengo la makala hii ni kujadili dhima za umatinishaji-upya wa matini zinazoakisi kipindi cha miaka ya 1970 katika muktadha wa miaka ya 2010. Matini hizo ni utendaji wa ngano tunayoweza kuiita “Posa” iliyotambwa na Mwalimu Nyerere katika sehemu za moja ya hotuba zake, na wimbo wa “Wahujumu na Walanguzi” ulioimbwa na *Asilia Jazz Band.* Matini hizi zilisambaa kwa kasi katika miezi ya mwanzo ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli. Katika mjadala huu, tutachambua maudhui ya matini teule kisha kufafanua dhima za matini hizi kumatinishwa-upya.

Mara baada ya kushinda kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwaka 2015, Rais Magufuli alichukua hatua kadhaa zilizoonesha matumaini kwa wananchi wengi. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa wakati huo ni kuonesha kwa vitendo nia yake ya kupambana na ufisadi ambao ulionekana kuwa kero kubwa kwa wananchi. Baada ya kuibua matatizo na kuanza kuyashughulikia ndani ya muda mfupi, wananchi walianza kuamini kuwa ufisadi ulianza kupata tiba mwafaka. Vilevile, hayati Rais Magufuli alisisitiza kuwa angewatetea wanyonge kwa hali na mali. Ili kuyafumbata barabara masuala haya, matini mbalimbali zikiwamo hotuba na nyimbo zilizohamasisha Sera ya Ujamaa na kuunga mkono Azimio la Arusha, hususani zile zinazojadili masuala ya unyonyaji zilisambaa katika mitandaopepe ya kijamii zikisadifu hali ya kupambana na ufisadi katika awamu ya Rais Magufuli, mchakato tuliouita umatinishaji-upya.

## 2.0 Umatinishaji-upya

Kwa kuwa mzizi wa dhana ya umatinishaji-upya ni matini, ni vema tukaanza kufafanua dhana ya matini kama inavyotumiwa katika makala hii. Matini ni dhana yenye utelezi mkubwa kwa sababu ina fasili nyingi. Aidha, si rahisi kupata fasili inayofumbata matumizi anuwai kwa sababu, wakati mwingine, dhana ya matini huhusishwa zaidi na lugha pekee, na wakati mwingine hujumuisha lugha na vipengele vingine vya kimasilugha (Radloff, 1993; Lotman, 1988). Dhana ya matini, ambayo imejadiliwa sana katika lugha ya Kiingereza, yaani *text* inatokana

na neno la Kilatini *textere* likimaanisha 'kufuma'. Istilahi hii imekuwa ikitumiwa kisitiari ikimaanisha mkusanyiko wa sentensi au matamshi yaliyofumwa kimuundo na kisemantiki yanayounda kitu kimoja kiushikamani na kimuwala (Wales, 2011). Dhana hii inatumika katika nyanja mbalimbali kama vile isimu, fasihi, anthropolojia na sosholojia (Beaugrande na Dressler, 1981). Nyanja hizi zina misingi tofauti ya kitaaluma. Ndiyo maana Lotman (1988) anadai kuwa matini ni dhana tata! Hata hivyo, mwanazuoni huyu anadai kuwa dhima kuu za matini ni kuwasilisha maana kwa uthabiti na kuzalisha maana mpya (Lotman, 1988).

Dhana ya matini inayoongoza mjadala huu ni ile iliyotolewa na William Hanks, anayedai kuwa "matini inaweza kufasiliwa kama mpangilio wowote wa alama ambazo zinaeleweka kimuwala (vyema) kwa baadhi ya watumiaji wake" (Hanks, 1989:95). Katika fasili hii, kuna dhana tatu za msingi: mosi ni alama. Alama inachukuliwa kwa mapana yake yote, yaani inajumuisha kifananishi, ishara na kionekezi – dhana zilizotolewa na mwanasemiotiki Charles Sanders Peirce (taz. Peirce na Hoopes, 1991); dhana ya pili ni muwala ambayo haitofautiani na ile inayotolewa na Michael Halliday na Ruqaiya Hasan kuwa uhusiano wa karibu wa vijenzi vya matini vinavyoleta maana (Halliday na Hasan, 2009); na dhana ya mwisho ni ya kisemantiki, yaani matini lazima ieleweke, isipoeleweka inapoteza dhana ya umatini. Baada ya kufafanua dhana hii ya matini, hatua inayofuata ni kufasili dhana ya umatinishaji-upya.

Umatinishaji-upya, kama ilivyodokezwa hapo juu, ni mchakato wa kuzidua[4] matini kutoka katika muktadha wake wa awali na kuichopeka katika muktadha mpya wa utendaji. Umatinishaji-upya unafumbata dhana kuu mbili, yaani usimuktadhishaji na umuktadhishaji-upya[5] (Bauman na Briggs, 1990). Usimuktadhishaji ni kitendo cha uchopoaji wa matini katika muktadha wake ili ibebeke na baadaye ichopekwe katika muktadha mwingine ambapo itamuktadhishwa upya. Umuktadhishaji-upya ni kitendo cha kuichopeka matini iliyochopolewa katika muktadha mpya ambapo inatambuliwa kama sehemu ya matini mpya. Wanazuoni hawa, Bauman na Briggs, wanasisitiza kuwa matini inapoziduliwa kutoka katika muktadha A, kwa vyovyote vile, inabeba baadhi ya nduni za muktadha A, nduni ambazo hudokezwa katika muktadha B. Mchakato huu wa umatinishaji-upya umezoeleka sana katika kazi za fasihi simulizi ambapo mtambaji huamua kuchukua kisa au motifu yoyote kati ya nyingi zilizomo katika gimba lake na kuichopeka katika muktadha mwingine pale anapoona inafaa. Greg Urban, miongoni mwa wanazuoni waliofafanua zaidi kuhusu dhana hii, anaongeza kuwa umatinishaji-upya huathiriwa na uhusiano baina ya yule anayeamua kumatinisha-upya matini na yule aliyeitoa matini husika. Vilevile, kuna uhusiano

[4] Mchakato wa kuondoa vipengele vya matini vinavyoweza kubebeka ili kuimuktadhisha katika muktadha mwingine. Ni kisawe cha neno la Kiingereza *extraction.*

[5] Visawe vya maneno ya Kiingereza *decontextualisation* na *recontextualisation* mtawalia.

wa karibu baina ya muktadha wa asili ambapo matini inasimuktadhishwa na ule inamomuktadhishwa-upya (Urban, 1996). Kwa ujumla, umatinishaji-upya ni suala linalofanyika katika kila jamii ambapo simulizi na tamaduni kutoka kizazi kimoja hurithishwa katika kizazi kingine katika miktadha tofauti (Silverstein na Urban, 1996).

### 2.1 Viwango vya Umatinishaji-upya

Ingawa waasisi wa dhana ya umatinishaji-upya, yaani Bauman na Briggs (1990) na Silverstein na Urban (1996) hawajaainisha bayana viwango vya umatinishaji-upya, Urban (1996) anadokeza kuwa umatinishaji-upya una viwango tofauti katika utendaji kulingana na mtazamo, hadhi na sifa na muktadha wa matini chanzi na ule unamomatinishwa upya. Suala hili linafanana na aina za udondoaji ambapo inaelezwa kuwa aina za udondoaji huukilia mtazamo, hadhi na sifa ya matini inayodondolewa na muktadha wa udondoaji (Fetzer, 2020). Kwa kuwa Urban (1996) na Fetzer (2020) wanadai kuwa kuna viwango mbalimbali vya umatinishaji na inaelezwa pia kuwa viwango hivyo vinadokeza mitazamo mbalimbali ya kimaudhui (taz. Fetzer na Weiss, 2020), katika makala hii tunapendekeza kuwa mchakato wa umatinishaji-upya uainishwe kwa viwango mbalimbali ili kubaini zaidi dhima zake. Kwa hiyo, kwa kuzingatia nduni zake bainifu, umatinishaji-upya umegawanyika katika aina kuu mbili, yaani umatinishaji-upya kamili, na umatinishaji-upya fifi.

#### 2.1.1 Umatinishaji-upya Kamili

Aina hii ya umatinishaji-upya huhusisha uziduaji wa matini yote bila kuchopoa vipengele kadha wa kadha na kuimukutadhisha katika muktadha mpya. Kuna sababu mbalimbali zinazochangia umatinishaji-upya kamili wa matini kama vile imani kwa matini chanzi. Kwa mfano, unukuzi wa matini mbalimbali za kidini katika miktadha mbalimbali huhusisha umatinishaji-upya kamili. Haya yanatokea kwa sababu mtu anayematinisha-upya dhana hizo ana imani kuwa matini hizo hazipaswi kubadilishwa chochote kutokana na utukufu wake. Matumizi ya semi mbalimbali katika jamii pia huhusisha umatinishaji kamili ili kurahisisha mawasiliano. Halikadhalika, katika uwanja wa sheria, hususani mahakamani, sheria mbalimbali hutajwa kama zilivyo ili kujenga hoja katika mivutano ya kisheria. Lengo kuu ni kuweka msisitizo kwa matini inayoziduliwa pamoja na kutimiza lengo la mmatinishaji kujiondoa katika matini hiyo (taz. Penfield, 1983; Yankah, 2012). Suala la umatinishaji-upya kamili limeingia na kushika kasi katika mitandaopepe ya kijamii kwani kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, masuala muhimu yanapozungumzwa hurekodiwa, husambazwa na wakati mwingine, hutumiwa ili kukidhi mahitaji ya miktadha mipya (Bublitz, 2015). Matini zinazojadiliwa katika makala hii ni za aina hii ya umatinishaji-upya kama itakavyofafanuliwa hapo baadaye.

### 2.1.2 Umatinishaji-upya Fifi

Umatinishaji-upya wa aina hii huhusisha utumiaji wa sehemu ya matini au vipande vya matini vilivyoziduliwa katika muktadha asilia na kuvimuktadhisha katika muktadha mpya. Sehemu au vipande hivyo huchanganywa na matini nyingine kulingana na mahitaji ya kimuktadha. Wakati mwingine, si rahisi kwa hadhira kubaini vipande vya matini vilivyomatinishwa; hivyo, maarifa makubwa huhitajika ili kubaini sehemu au vipande vya matini vilivyomatinishwa-upya. Kama ilivyo katika umatinishaji-upya kamili, aina hii ya umatinishaji-upya ina sababu zake. Baadhi ya sababu hizo ni kuepuka kurudia matini ndefu kupita kiasi ambapo njia pekee ya kuirejelea ni kuchukua baadhi ya vipande muhimu vya matini hiyo, na hususani wazo kuu. Vilevile, sababu nyingine ni kutokuichukulia matini kwa uzito mkubwa kwa sababu mbalimbali. Inawezekana mmatinishaji-upya haamini sana umahiri wa anayetoa matini chanzi kwa sababu mmatinishaji-upya ana uelewa wa kutosha kuhusu matini husika (taz. Urban, 1996). Aidha, wakati mwingine, mtendaji hutumia umatinishaji-upya fifi kwa sababu ya kukosa kumbukumbu au uhakika wa matini chanzi kama ilivyodokezwa katika utambaji wa ngano ya "Posa" uliofanywa na Mwalimu Nyerere.

Umatinishaji-upya unaojadiliwa katika makala hii ni kamili, yaani matini zimeziduliwa kama zilivyo na kumuktadhishwa katika muktadha mpya bila kubadilishwa chochote. Hili limechangiwa na maendeleo ya kiteknolojia ambapo matini teule, yaani ngano na wimbo vilivyorekodiwa wakati huo na kuhifadhiwa, vilisambazwa katika mitandaopepe ya kijamii mwaka 2016.

## 2.2 Umatinishaji-upya wa Matini Zilizorekodiwa

Katika makala hii, ni muhimu kutatua changamoto mbili za kinadharia kabla ya kufanya uchambuzi: mosi, utendekaji wa matini zilizokwisharekodiwa, na pili, utendaji wa matini hizo katika mitandaopepe ya kijamii. Sababu ya kuzitatua changamoto hizi kabla ya kujadili umatinishaji-upya inatokana na misingi ya umatinishaji-upya iliyokitwa zaidi katika utendaji, sifa inayoipa uhai fasihi simulizi. Ni muhimu kuelewa kuwa misingi ya kijadi ya utendaji inakita mizizi yake katika kuwapo kwa fanani na hadhira pahala pamoja, yaani pande hizo mbili zionane ana kwa ana: aina hii ya utendaji imekuwapo katika jamii zote duniani (Auslander, 2008). Mtagusano huu wa ana kwa ana ndio unaomwezesha fanani kuwasiliana na hadhira kutoka mwanzo hadi mwisho wa tukio (Bauman, 1975; 2012).

Hata hivyo, kuna changamoto mbili zinajitokeza katika umatinishaji wa matini simulizi ambazo zilirekodiwa ambapo msikilizaji, pamoja na kuelewa dhamira ya ujumbe kulingana na muktadha, analazimishwa kuelewa kuwa matini hiyo iliziduliwa katika muktadha fulani. Inaelezwa kuwa mabadiliko ya kiteknolojia yamesababisha baadhi ya wanazuoni kupanua wigo wa utendaji kutoka kuonana ana kwa ana hadi kujumuisha mawasiliano ya kidijiti kama vile intaneti (Wunderer, 1999), runinga na muziki uliorekodiwa (Auslander, 2008).

Kwa hiyo, matini teule, yaani ngano na wimbo, kwa mantiki hiyo, vinaweza kusikilizwa katika kifaa chochote na kuchukuliwa kuwa ni sehemu ya utendaji wa kazi za fasihi simulizi. Auslander (2008) anaeleza kuwa utendaji-mubashara una tofauti ndogo sana na utendaji-bebezi[6] kwa sababu tofauti za kuibua hisia baina ya pande hizi mbili ni ndogo sana. Davis (2012) anaendeleza mjadala huu kwa kusisitiza kuwa, umubashara na ubebezi pekee si suala la msingi katika kutofautisha dhana hizi mbili, badala yake, msingi mkubwa uwekwe katika uibuaji wa hisia miongoni mwa hadhira na washiriki kwani hii ndiyo athari iipatayo hadhira. Pamoja na msisitizo wa ubunifu wa vifaa vya kisasa, Davis (2012) anadai kuwa wavumbuzi katika eneo la utendaji wajikite katika malengo, maudhui na ubora wa vifaa na uibuaji wa hisia kwa hadhira. Kwa mantiki hiyo, wimbo na ngano teule vinaweza kuchunguzwa na kutathminiwa kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Utendaji kwa sababu katika muktadha wa mitandaopepe ya kijamii kama vile *WhatsApp*, matini hizi zinachukuliwa kama sehemu ya utendaji.

Usambazaji wa ujumbe wa kifasihi kama muziki, video, simulizi fupifupi za maigizo ya aina mbalimbali kama vile ucheshi, mahubiri au mafunzo kadha wa kadha katika apu ya *WhatsApp*, kwa kuzingatia hoja zilizotolewa hapo juu, ni aina mojawapo ya utendaji ambapo washiriki katika kundi ni hadhira ambayo hushiriki kwa kutoa maoni. Kama ilivyoelezwa na Davis (2012) kuwa msingi mkubwa wa utendaji uwekwe katika uibuaji wa hisia na vionjo mbalimbali, ujumbe wa simu pamoja na media zake zote husambazwa kwa kuzingatia umuhimu na thamani ya maudhui, utambulisho wa kijamii na hisia za msomaji (Bakare, Abdurrahaman na Owusu, 2022). Kwa hiyo, hisia na vionjo hutawala katika utendaji wa matini, upokezi na hatimaye huhamasisha wasomaji hao kuwasambazia wengine. Kama ilivyo katika utendaji (taz. Bauman, 2012), uamuzi wa kutuma kwa wengine kazi yoyote ile ya kisanaa unahusishwa na namna mtumaji alivyojinasibisha katika kundi sogozi; sababu kubwa ni kwamba media inayotumwa inaweza kumdhalilisha na kumuondolea utu wake ingawa si yeye aliyeitengeneza. Kwa hiyo, msambazaji wa ujumbe ni kama vile meneja wa sanaa inayotumwa katika kundi sogozi. Mitandaopepe ya kijamii kwa mantiki hiyo ni jukwaa mbadala la utendaji (Wunderer, 1999) na sehemu ya wazi kama inavyosisitizwa na (Hadley, 2017:14):

> *I cast social media platforms as a part of the public sphere, by which I mean the shared space or place—conceptual rather than concrete—in which new ideas about identity, society, social institutions and their meanings are negotiated.*
>
> Ninachukulia majukwaa ya mitandaopepe kama sehemu ya wazi, maana yake eneo ambalo linatumiwa na wote—kidhanifu zaidi kuliko kimaumbile—ambapo mawazo mapya kuhusu utambulisho, jamii, asasi za kijamii na maana zake zinajadiliwa (Tafsiri yangu).

[6] Kisawe cha neno la Kiingereza *mediated performance*.

Aidha, inaelezwa kuwa ili taaluma ya fasihi simulizi iendelee, ni lazima izingirishwe[7] katika mitandao ya kijamii, vinginevyo, taaluma ya fasihi simulizi itazidi kuwa finyu na hatimaye itakufa kabisa (Mnenuka, 2019). Kwa hiyo, kazi mbalimbali za fasihi simulizi, zikiwamo zilizorekodiwa zinapaswa kuchambuliwa kwa kuzingatia misingi yote ya fasihi simulizi.

Ingawa imeelezwa kuwa utendaji katika makundi sogozi unaelekea kufanana na utendaji wa kawaida, swali muhimu katika mjadala huu ni hili, je, makundi sogozi ya *WhatsApp* na mitandao mingine ni majukwaa ya kisanaa kiasi cha kuwafanya washiriki kuwa hadhira? Kama yalivyo makundi ya kawaida katika jamii, makundi sogozi hujadili masuala mbalimbali yanayowahusu na masuala mengine ya kijamii ikiwamo kusambaza ujumbe wa aina mbalimbali bila kukiuka misingi waliyojiwekea. Miongoni mwa ujumbe unaosambazwa ni kazi za kisanaa. Kwa hiyo, washiriki katika makundi sogozi hugeuka kuwa hadhira pale wanapotazama au kusikiliza kazi za kisanaa. Aghalabu, utendaji wa sanaa katika jamii una ugiligili kwa kiasi kikubwa kwani huweza kutokea hata nje ya tukio rasmi la kisanaa. Kwa hiyo, matukio ya kisanaa katika maisha ya kila siku ni ya muda mfupi ambayo huibuka na kupotea bila kutarajiwa (Mnenuka, 2021). Kwa mfano, utendaji wa utani miongoni mwa wanajamii hutokea na kupotea katika mazingira ya kazi, misiba, furaha na kadhalika wakati mwingine bila kutabirika. Kwa mantiki hiyo, mara kwa mara, majukwaa sogozi hugeuka kuwa majukwaa ya kisanaa pale kunapoibuka utani na tanzu nyingine za kifasihi au pale zinapotumwa kazi za kisanaa ambapo zinaweza pia kuibua mijadala kuhusu maudhui yaliyomo.

## 3.0 Matini Teule

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya utangulizi, matini zilizolengwa katika uchunguzi huu ni ngano ya "Posa" iliyotambwa na Mwalimu Nyerere na wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" ulioimbwa na *Asilia Jazz Band*. Kabla ya kuchambua dhima za matini teule, sehemu hii itajadili kwa muhtasari utendaji wa matini hizo katika muktadha wake asilia.

### 3.1 Ngano ya "Posa"

Inasimuliwa kuwa kulikuwa na msichana mzuri anayetaka kuolewa. Msichana huyu alikuwa akiishi kilimani. Chini ya kilima hicho kulikuwa na ajuza ambaye alitoa sharti la kumfikia msichana huyo. Sharti hilo lilikuwa kutokugeuka nyuma hata kama kungesikika sauti na vishindo vya kutisha. Vijana wengi walijaribu lakini walishindwa kwani hawakuwa na ujasiri wa kutokugeuka pale kelele hizo zilipozidi kuwatia hofu. Yeyote aliyegeuka alibadilika na kuwa jiwe. Kijana mmoja mdogo na mzuri, ambaye alidhamiria kumuoa msichana huyo, hakugeuka na alifanikiwa kumfikia msichana huyo, na hatimaye, alimuoa. Kisha akarudi akiyanyunyizia dawa yale mawe ambayo yaligeuka tena kuwa watu kama hapo

[7] Kuwekwa kwa namna inayoendana na suhula na mazingira.

awali. Kisha mtambaji anamalizia kwa kusisitiza kuwa yeye ataendelea na msimamo wake wa kutetea haki bila kutishwa na kelele anazozikisia.

### 3.2 Wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi"

Wimbo huu unaeleza kuwa hatua za kuwashughulikia wahujumu na walanguzi zimeanza kuchukuliwa. Hatua hizo zimetajwa kitaswira kama "bomu lililolipuka". Inaelezwa namna wahujumu na walanguzi walivyosababisha wananchi kuwa na maisha magumu kwani bidhaa mbalimbali za msingi zilipotea sokoni kwa sababu zilifichwa. Mwishoni, serikali inaanza kuwachukulia hatua, "bomu limelipuka" na wananchi wanahamasishwa kuwafichua wahujumu uchumi na walanguzi ili kuiunga mkono serikali iliyotia nia ya kupambana na watu hao waliokuwa na nia mbaya.

## 4.0 Dhima za Umatinishaji-upya

Katika muktadha wa makala hii, dhana ya umatinishaji-upya ambayo imetumika pia kama kiunzi cha kiuchambuzi ina dhima mbalimbali kama vile kudokeza mamlaka ya mhusika wa matini asilia, kuibua kumbukumbu ya pamoja ya nchi, kuongeza ustawi wa jamii, na mwisho katika mjadala huu ni kuongeza ujasiri na hamasa kwa uongozi.

### 4.1 Kudokeza Mamlaka ya Mhusika wa Matini Asilia

Kwa kawaida, lengo kubwa la kumatinisha-upya matini ni kukubali ukuu na umuhimu wa matini iliyoziduliwa kutokana na heshima na ukuu wa aliyeitoa kauli hiyo au kinyume chake. Na huu ndio msingi wa kumuktadhishwa-upya katika mazingira tofauti. Katika utambaji wa ngano[8] teule katika hotuba ya Mwalimu Nyerere, msingi mkubwa wa umuhimu huo unajitokeza pale anapofafanua maana ya ngano hiyo, yaani kutokutetereka kwa msimamo wake wa kutetea wanyonge wala kutishwa na sauti yoyote ile kama anavyonukuliwa:

> Na mimi ni... nasema kama nazisikia hizo kelele sasa hivi... kama nazisikia, zingine hapahapa Tanzania, zingine kutoka nje ya Tanzania, "Haooo... haooo... wamekosea njia... haooo... haoo... wachinje..." Sasa Watanzania, mimi sikubali kuwa jiwe. Sasa kama ukisema ni woga au nini, potelea mbali. Lakini kuwa jiwe sikubali hata kidogo! Sigeuki nyuma... (makofi). Maana ama tulikusudia kweli ama tulitania. Ama tulikusudia kweli kujenga nchi ya Uja... haki ama tulikuwa tunatania tu! Sasa kama tulikusudia, hatuwezi kurudi nyuma kwa kelele za wapumbavu na wanyonyaji. Tutakwenda tu! Tutapata matatizo, tutapata majizi humuhumu, tutatapa wanyang'anyi humuhumu,

[8] Katika fasihi simulizi, kila atendaye kazi ya fasihi simulizi, hususani ngano katika muktadha huu, ana sifa zote za kuwa fanani. Kwa hiyo, hakuna fanani asilia na fanani bebezi (*mediated performer*). Kwa mantiki hiyo, Nyerere ni mtendaji wa ngano hiyo hata kama anaanza kwa kudai kuwa hakikumbuki vizuri kisa cha ngano husika.

> mtapata watetezi wa mabepari humuhumu. Watazidisha kelele lakini tutakwenda. Wanaotaka kugeuka mawe, geukeni. (kicheko).

Hiki ndicho kiini cha utendaji wa ngano hii ya "Posa". Mamlaka na ukuu wa simulizi hii unatokana na kiini hiki ambacho kila mwananchi anatamani kukiona, yaani misimamo ya kiongozi mwadilifu (Ciulla, 2005) ambaye yupo mstari wa mbele kuwasaidia wananchi. Hotuba hiyo haikujulikana kwa wengi kwa miaka mingi bali iliibuka ndani ya miezi miwili ya urais wa hayati Rais Magufuli. Ukiwaweka pamoja, katika muktadha wa Tanzania, Nyerere, Baba wa Taifa, anaonekana kuwa na mamlaka na ushawishi mkubwa kisiasa[9] kuliko Rais Magufuli. Mamlaka, ukuu na ushawishi mkubwa wa kisiasa wa Mwalimu Nyerere unatokana na uadilifu wake kama inavyoelezwa hapa chini:

> *Nyerere has been sub-Saharan Africa's most acclaimed political Prophet and perhaps the best example of the moral agent in political history… Nyerere is a teacher of socialist morality—and of a socialism infused with Christian ethics. In the eyes of many he has become the moral leader of Africa, and to some extent of the Third World as a whole.* (Jackson na Rosberg, 1982:221)

> Nyerere amekuwa kiongozi anayetazamwa kama Nabii wa siasa na labda mfano bora kabisa wa mtu mwenye uadilifu uliotukuka katika historia ya siasa… Nyerere ni mwalimu wa uadilifu wa kijamaa—na wa ujamaa ulioathiriwa pia na maadili ya Kikristo. Kwa mtazamo wa watu wengi amekuwa kiongozi wa uadilifu wa Afrika, na kwa kiasi fulani wa nchi zote zinazoendelea kwa ujumla (Tafsiri yangu).

Kwa hiyo, kuenea na kusambaa kwa ngano hiyo, ambayo ni sehemu ya hotuba ya Rais Nyerere kunaonesha kuwa suala lililokuwa likifanywa na Rais Magufuli limepigwa mhuri na mtu mwenye mamlaka na ushawishi mkubwa wa kisiasa nchini Tanzania. Kimsingi, ilimaanisha aendelee kufanya hayo anayoyafanya. Inaelezwa kuwa, mara alipoingia madarakani, hayati Magufuli alitekeleza baadhi ya ahadi zake za uchaguzi kwa namna ambayo iliwashangaza si tu Watanzania bali raia wa nchi mbalimbali barani Afrika (Anudo, Rotumoi na Kodak, 2021). Rais Magufuli alianza kutekeleza ahadi zake za uchaguzi kwa kupambana na ufisadi, kuboresha usimamizi na kurekebisha baadhi ya sheria za kodi, kuimarisha ukusanyaji wa kodi, kupambana na umaskini, kununua vitanda vya hospitali na kudhibiti utapanyaji wa fedha za umma – matatizo yanayolikumba bara la Afrika (Bamwenda, 2019). Kwa mfano, mtoa-maoni mmoja katika ukurasa wa *YouTube* ambamo ngano hiyo iliyotambwa na Nyerere imepakiwa anasema, "Tutakukumbuka sana mwendazake Mwalimu Nyerere tunafurahi hayati Magufuli

[9] Akizungumza katika kipindi cha "Mikasi", Tundu Lissu aliyekuwa mbunge, alisema kuwa hadhi ya Nyerere kwa baadhi ya Watanzania imefikia kulinganishwa na muungu akitumia neno la Kiingereza *demigod* (Jabir na Murunga, 2015).

alishika nyayo zako Baba Mungu awalaze mahali pema peponi. Amina. Tutawakumbuka daima" (TZBN Online, 2018). Kwa baadhi ya watu, huu ulikuwa mwanzo mzuri ulioanza kufanana na yale yaliyosisitizwa na Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata baada ya kung'atuka. Msimamo wake ulilenga kuwakutetea wanyonge na kujali utu.

**4.2 Kuibua Kumbukumbu ya Pamoja ya Nchi**

Mwanzoni mwa utawala wa Rais John Magufuli, umatinishaji-upya wa matini teule ulikuwa na dhima ya kuibua kumbukumbu ya pamoja ya nchi ya Tanzania. Kumbukumbu si mchakato wa kuchukua na kutumia data iliyohifadhiwa akilini tu bali ni mchakato ulio hai kwa sababu kumbukumbu huibuliwa na kuhusishwa na masuala yanayofikiriwa au kujadiliwa kwa wakati husika. Binadamu hakumbuki kila kitu kwa wakati wote, bali hukumbuka yale tu yanayohusiana na masuala anayoyashughulikia wakati huo; halikadhalika, kumbukumbu hutumiwa ili kusaidia kujenga au kutatua suala fulani linalohusika (Brace na Roth, 2002; Vaz da Silva, 2012).[10] Kwa hiyo, matendo yaliyokuwa yakifanywa na Rais Magufuli ndiyo yaliyoibua kumbukumbu kuhusu wimbo teule na ngano ya kugeuka jiwe. Kwa namna ya pekee, nyimbo huibua kumbukumbu mbalimbali ukiwamo wimbo wenyewe. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa nyimbo huibua kumbukumbu hata zile ambazo kwa hali ya kawaida mtu asingezikumbuka (Bryant, 2005; Wilson Jr., 2006). Kwa mfano, Bryant (2005) alipokuwa akiwahoji watoataarifa kuhusu Mapinduzi ya Kitamaduni nchini China ambao walishindwa kusimulia masuala mengi yaliyotukia wakati huo, baada ya kuwasomea matini za nyimbo mbalimbali, watoataarifa hao walieleza masuala mbalimbali kuhusu matukio, hisia na kumbuhisi[11] zinazohusiana na mapinduzi hayo. Kama Byant (2005), Wilson Jr. (2006) anadai kuwa nyimbo ziliwasaidia watoataarifa wake kuibua kumbukumbu za masuala mbalimbali yaliyotukia walipokuwa wadogo. Kwa hiyo, nyimbo ni nyenzo muhimu katika kuibua kumbukumbu, hisia na kumbuhisi.

Matini teule katika makala hii zililenga kuibua kumbukumbu ya Rais Nyerere sambamba na misimamo yake ya kupigania haki na zaidi harakati za kupambana na wahujumu uchumi. Wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" uliibua kumbukumbu ya muktadha unaofanana na huo. Wakati huo, serikali ilidhamiria kushughulikia tatizo la uhujumu uchumi na ulanguzi wa bidhaa mbalimbali. Tatizo hilo liliwanufaisha baadhi ya watu na kuwaumiza watu wenye uwezo mdogo. Katika wimbo huu, mwimbaji anaeleza ugumu wa maisha unavyosababishwa na

[10] Ni muhimu kukumbuka kuwa masuala haya si mageni sana miongoni mwa wanazuoni kwani yameshajadiliwa kwa kina. Kwa mfano, katika utafiti wake Frederic C. Bartlett alibaini kuwa binadamu hukumbuka pale anapohitaji kuitumia kumbukumbu katika kubaini suala fulani (Bartlett, 1995). Kwa hiyo, naye alisisitiza kuwa taarifa mbalimbali hazihifadhiwi sehemu fulani kama ghala ili zichukuliwe zinapohitajika bali zipo hai na hujitokeza katika muktadha wowote mwafaka.

[11] Neno hili linatumika kama kisawe cha neno la Kiingereza *nostalgia*.

wahujumu uchumi na walanguzi kama baadhi ya maneno ya wimbo huo yalivyonukuliwa:

*Kila nilichofanya,*
*Sijui kilikokwenda,*
*Kazi nilifanya,*
*Mshahara nilipata oooh*
*Oooh maisha magumu eeh! x 2*
*Nilikuwa na wake wawili,*
*Mmoja nimeshamuacha,*
*Sababu ya matatizo,*
*Maisha yalipanda aah!*
*Sababu ya hao walanguzi eeh! x 2*

*Nikilala nikiamka aah!*
*Unga hauonekani.*
*Nikilala nikiamka aah!*
*Sukari haionekani*
*Nikilala nikiamka aah!*
*Sabuni haionekani,*
*Nikilala nikiamka aah!*
*Mchele hauonekani.*
*Kumbe sababu ya walanguzi eeh!*

Watu waliowahi kuzisikia nyimbo na hotuba hizi, wanapozisikia nyimbo na hotuba teule, hukumbuka masuala mengi na kuyahusisha yale yalizokuwa yakitukia mwaka 2016. Katika muktadha mpya, wananchi walipata changamoto za ugumu wa maisha kwa sababu ya ufisadi uliowanufaisha wachache huku wengi wakiumia (Bamwenda, 2019). Nyerere ana hotuba nyingi na kuna miziki mingi inayohamasisha uzalendo na inayopiga vita unyonyaji na uhujumu uchumi; kwa nini kipande hiki tu cha hotuba ya Mwalimu Nyerere na wimbo huu? Kwa mujibu wa Rolston (2010), kumbukumbu za matukio yaliyopita zinaweza kuathiri matendo ya leo. Kwa hiyo, kwa kutumia hotuba, wasikilizaji walipata msimamo wa serikali kuhusu haki za raia, na katika wimbo teule, jamii katika muktadha wa pili, nyakati za Rais Magufuli ilipata mtazamo wa wananchi wa wakati huo. Kwa mfano, mmoja wa waliotoa maoni kuhusu wimbo huu wa "Wahujumu na Walanguzi" kwenye mtandao wa *YouTube* anahusisha maudhui yanayoimbwa katika wimbo huo na juhudi zilizofanywa na Rais Magufuli katika kupambana na vitendo vya kifisadi. Mtoa-maoni huyo anasema, "Huu wimbo wa kitambo ila juhudi za Rais wa sasa wa awamu ya tano J.P.M. anavyopambana na mafisadi hapa huu wimbo ni mahali pake *well done* JPM" (Nassor, 2018).

Aidha, "kumbukumbu huibuliwa ili kuponya, kulaumu na kuhalalisha" (Antze na Lambek, 1996: xii). Katika muktadha huu, kumbukumbu ya wimbo na ngano iliibuliwa ili kwa upande mmoja, iponye majeraha ya kisaikolojia na kimaumbile yaliyotokana na ufisadi na kuwakosesha wananchi huduma bora za afya. Kwa upande mwingine, kumbukumbu ya matini teule iliibuliwa ili kuhalalisha jitihada zilizokuwa zikifanywa na Rais Magufuli. Aidha, kumbukumbu hii ililenga kuwakumbusha watu kuwa nchi iliwahi kupitia changamoto zilizofanana na kukithiri kwa vitendo vya kifisadi na wananchi waliungana na serikali ili kupambana na vitendo vya ukiukaji wa haki.

### 4.3 Kuongeza Ustawi wa Jamii

Baada ya kukithiri kwa vitendo vya kifisadi hadi mwishoni mwa miaka ya 2015, hatua zilizoanza kuchukuliwa na Rais Magufuli zilianza kuwatia moyo raia na

kutoa matumaini ya vitendo hivyo kupungua katika jamii. Kwa mujibu wa Bamwenda (2019), miongoni mwa masuala yaliyomwinua Rais Magufuli ni pamoja kupiga vita ufisadi ulioonekana kuwakera raia wengi. Inaelezwa kuwa ufisadi hupunguza au hudhoofisha ustawi wa mtu (Sulemana, Iddrisu na Kyoore, 2017). Hali ya kudhoofisha ustawi wa jamii hupunguza furaha pia kwa sababu raia hukosa huduma bora kama wanavyostahili na kwa kiasi kikubwa kukosa uhakika wa kupata huduma. Baadhi ya wanazuoni wanadai kuwa kukosa uhakika wa masuala kadha wa kadha katika maisha hupunguza ustawi kwa ujumla wake (Witte, 1999; Scholarios, Hesselgreaves na Pratt, 2017). Kwa mfano, wakati Witte (1999) anadai kuwa kukosa uhakika wa kazi (ajira) hupunguza ustawi wa mtu kisaikolojia; Scholarios, Hesselgreaves, na Pratt (2017) wanadai kuwa kutokutabirika kwa muda wa kazi kwa wafanyakazi hupunguza ustawi wa maisha. Kutokutabirika kwa huduma za umma kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ufisadi kulipunguza ustawi wa maisha na furaha pia. Kwa hiyo, vitendo vilivyokuwa vikifanywa na Rais Magufuli vilikuwa vinatoa matumaini ya ustawi mpya wa jamii kwani baadhi ya raia waliamini kuwa vitendo vya kifisadi vilikuwa vikielekea ukingoni. Kwa hiyo, matumaini hayo yalidhihirishwa na kusambazwa kwa wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" pamoja na ngano iliyotambwa na Nyerere kama msisitizo wa kuonesha kuwa ataipigania haki bila kujali kelele zinazomkatisha tamaa. Umatinishaji-upya wa matini hizi katika muktadha huu ulitokana na furaha ya matendo yaliyokuwa yakiendelea ya kupambana na vitendo vya ufisadi kutoa matumaini ya ustawi mpya wa jamii. Kwa hiyo, wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" ulikuwa kama kejeli na dhihaka kwa mafisadi kwamba "…bomu limeshapasuka" na wao wapo katika hali tete.

### 4.4 Kuongeza Ujasiri na Hamasa kwa Uongozi

Kihistoria, nyimbo zimetumiwa katika matukio mengi kama nyenzo ya kuongeza ujasiri na hamasa, hasa katika mazingira ambapo kuna uwezekano mkubwa wa watu kukata tamaa kama vile katika kazi au vita (Chiwome, 1990; Wilson Jr., 2006; Nuxoll, 2014). Chiwome (1990) anaeleza jinsi nyimbo zilivyotumika nchini Zimbabwe katika vita vya ukombozi. Dhima kubwa ya nyimbo hizo ilikuwa: mosi, kukuza urazini wa ubaya wa ukoloni; pili, kuonesha nia ya kutotii, kuibua matumaini, kuondoa woga, kuleta furaha na uchungu; tatu, kutunza historia ya mageuzi makubwa ya kijamaa, na mwisho ni kuwatia moyo wapiganaji. Pamoja na dhima nyingine zinazofanana na zile zilizofafanuliwa na Chiwome (1990), Wilson Jr. (2006) anadai kuwa, katika kipindi cha ukoloni wa Waingereza katika koloni la Kenya, nyimbo zilitumika kama nyenzo ya kuwatia ujasiri Wakenya katika kipindi kigumu ilipotangazwa hali ya hatari wakati wa ukoloni wa Waingereza. Aidha, Nuxoll (2014) anaeleza dhima za nyimbo wakati wa vita vilivyopiganwa nchini Sierra Leone miaka ya 1990. Mwandishi anadai kuwa nyimbo hizo zilikuwa na dhima ya kuwatia moyo na ujasiri wapiganaji.

Katika muktadha wa Tanzania mwaka 2016, wimbo wa “Wahujumu na Walanguzi” ulitumika kama nyenzo ya kuwahamasisha viongozi katika serikali ya Magufuli kuendeleza mapambano katika vita dhidi ya wahujumu uchumi na mafisadi. Kipande chenye msisitizo zaidi ni kile chenye maneno yanayosisitiza:

*Sasa vita imetangazwa jama,*
*Wananchi wote tuwe imara.*
*Sasa vita imetangazwa jama,*
*Wananchi wote tuwe imara.*
*Vijijini na mijini, tusisite kuwafichua,*
*Wahujumu na walanguzi.*
*Vijijini na mijini, tusisite kuwafichua,*
*Wahujumu na walanguzi.*

Kitendo cha kusambaza matini katika mitandaopepe ya kijamii kilitokana na baadhi ya watu kuguswa na maudhui ya wimbo huu sambamba na kukubaliana na ujumbe wake kama inavyoshadidiwa na wanazuoni mbalimbali (taz. Bakare, Abdurrahaman na Owusu, 2022). Kiwango cha kusambaa kinatokana na wengi kuguswa na hotuba na wimbo teule. Kwa hiyo, dhima mojawapo ya umatinishaji-upya wa matini teule katika muktadha wa uongozi wa hayati Rais Magufuli ni kuwatia ujasiri viongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na mafisadi kwa kile alichokiita “utumbuaji wa majipu”, hatua ambazo zinafanana na zile zilizofanywa na Mwalimu Nyerere na kuimbwa kama “bomu lililolipuka ili kuwasambaratisha wahujumu uchumi na walanguzi”. Aidha, hotuba, kama ilivyokuwa kwa nyimbo, husambazwa kwa malengo yaleyale ya kuwatia moyo wale wanaoelekea kukata tamaa, hususani katika muktadha huu wale waliokuwa wakipambana na ufisadi. Kwa mfano, Mwalimu Nyerere alipokuwa akifafanua maana ya ngano husika alisema, “Sasa kama ukisema ni woga au nini, potelea mbali. Lakini kuwa jiwe sikubali hata kidogo! Sigeuki nyuma...”.

Kipande hicho cha ngano na tafsiri yake vilisambazwa ili kuwatia moyo viongozi wa serikali ya Rais Magufuli waliokuwa wakipambana na ufisadi. Hili linaelezwa pia na Raphael Kibiriti aliyeandika makala gazetini ili kumuunga mkono na kumtia moyo Rais Magufuli kuendelea na mapambano ya ufisadi kama anavyosema:

> Katika moja ya hotuba alizowahi kuzitoa baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kuna ile ilizungumzia mtu aliyegeuka jiwe baada ya kuangalia nyuma kutokana na kelele nyingi za kumzomea. ...Ni rai ya makala hii kwa Dk. Magufuli, kutogeuka nyuma kutokana na zomea zomea inayojitokeza dhidi ya msimamo wake wa kuipeleka nchi mbele, na badala yake akaze uzi, ahakikishe kuwa wembe ni ule ule (Kibiriti, 2016).

Dondoo hili linadhihirisha mitazamo ya baadhi ya watu waliokuwa wakiunga mkono jitihaza za Rais Magufuli katika vita vyake dhidi za ufisadi na kuwatetea

wanyonge. Mwandishi amejenga hoja yake kwa kutumia ngano iliyotambwa na Mwalimu Nyerere kwa lengo la kuwatia ujasiri viongozi wa Awamu ya Tano.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala hii, dhana ya umatinishaji-upya, kama dhana ya kiuchambuzi imetumiwa kujadili umuktadhishwaji-upya wa matini mbili, ngano iliyotambwa na Mwalimu Nyerere kama sehemu ya hotuba yake na wimbo wa "Wahujumu na Walanguzi" ulioimbwa na bendi ya *Asilia Jazz Band*. Matini hizo zilisambazwa kwa njia mbalimbali za mitandaopepe, hususani katika makundi sogozi ya *WhatsApp*. Tumejadili namna matini hizi zinavyochukuliwa kama sehemu ya utendaji wa fasihi simulizi ambapo mara kwa mara majukwaa sogozi hugeuka kuwa majukwaa ya kisanaa.

Kuhusu matini teule, tumeona kuwa pamoja na matini hizi kutumiwa zaidi ya miaka thelathini iliyopita katika kuhamasisha watu kupambana na wahujumu uchumi na walanguzi ili kupunguza ugumu wa maisha, zimetumiwa kama chachu ya kuhamasisha jitihada za kupambana na ufisadi. Katika makala hii, tumejadili pia dhima za umuktadhishaji-upya wa matini hizo katika urais wa Magufuli mwanzoni mwa mwaka 2016. Dhima zilizojadiliwa katika makala hii ni udokezaji wa mamlaka ya aliyetoa hotuba, yaani Nyerere, kuibua kumbukumbu, kuongeza ustawi wa jamii na kuongeza hamasa na ujasiri kwa wapigania haki.

## Marejeleo

Alfaro, M.J.M. (1996). "Intertextuality: Origins and Development of the Concept." *Atlantis*. Juz. 18 (1/2): 268–85.

Antze, P. na Lambek, M. (1996). "Introduction: Forecasting Memory". Katika P. Antze na M. Lambek (Wah.), *Tense Past: Cultural Essays in Trauma and Memory*. New York: Routledge. Kur. xii–xxxviii.

Anudo, C., Rotumoi, J., na Kodak, B. (2021). "We Choose to See No Evil: John Pombe Magufuli, the Nationalist Who Championed the Sovereignty of His Country." *Journal of African Studies and Ethnographic Research*. 3(3): 43-61. Inapatiakana katika https://royalliteglobal.com/african-studies/article /view/682. Ilisomwa tarehe 15/11/2022.

Auslander, P. (2008). "Live and Technologically Mediated Performance". Katika T.C. Davis (Mh.), *The Cambridge Companion to Performance Studies*. Cambridge: Cambridge University Press. Kur. 107-119.

Bakare, A.S., Abdurrahaman, D.T. na Owusu, A. (2022). "Forwarding of Messages Via WhatsApp: The Mediating Role of Emotional Evocativeness". *Howard Journal of Communications*. Juz. 33(3):265-280. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/10646175.2021.1974611 .Ilisomwa tarehe 18 Januari 2022.

Bakhtin, M.M., Holquist, M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays, University of Texas Press Slavic Series*. Austin: University of Texas Press.

Bamwenda, E. (2019). "The Symptoms of the Shift towards an Authoritarian State in Tanzania's President John Pombe Magufuli's Rule." *Politeja*. 15:123–150. Inapatikana katika https://doi.org/10.12797/Politeja.15.2018.56.08

Barber, K. (2007). *The Anthropology of Texts, Persons and Publics [Oral and Written Culture in Africa and Beyond]*. Cambridge; New York: Cambridge University Press.

Bartlett, F.C. (1995). *Remembering: A Study in Experimental and Social Psychology*. New York: Cambridge University Press.

Bauman, R. (1975). "Verbal Art as Performance." *American Anthropologist, New Series.* Juz. 77: 290–311. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/674535. Ilisomwa tarehe 10 Oktoba 2020.

Bauman, R. (2012). "Performance". Katika R. Bendix na G. Hasan-Rokem (Wah.), *A Companion to Folklore*. *Blackwell Companions to Anthropology*. Malden, MA: Blackwell. Kur. 93-118.

Bauman, R. na Briggs, C.L. (1990). "Poetics and Performance as Critical Perspectives on Language and Social Life." *Annual Review of Anthropology.* Juz. 19: 59-88.

Beaugrande, R. na Dressler, W. (1981). *Introduction to Text Linguistics*. London na New York: Longman. Kimechapishwa tena mkondoni na kinapatikana katika anwani hii http://library.lgaki.info:404/2017/De%20Beaugrande %20R.-A..pdf.

Blommaert, J. (1999). *State Ideology and Language in Tanzania*. Cologne: Rüdiger Köppe.

Blommaert, J. (2005). *Discourse: A Critical Introduction*. Cambridge, UK: Cambridge University Press.

Brace, N. na Roth, I. (2002). "Memory: Structures, Processes and Skills". Katika D. Miell, A. Phoenix, K. Thomas (Wah.), *Mapping Psychology 2*. Milton Keynes: Open University. Kur. 111-169.

Bryant, L.O. (2005). "Music, Memory, and Nostalgia: Collective Memories of Cultural Revolution Songs in Contemporary China." *China Review, Special Issue on Collective Memories of the Cultural Revolution*. Juz. 5: 151-175.

Bublitz, W. (2015). "Introducing Quoting as a Ubiquitous Meta-Communicative Act." Katika J. Arendholz, W. Bublitz, M. Kirner-Ludwig (Wah.), *The Pragmatics of Quoting Now and Then*. Berlin: De Gruyter Mouton. Kur. 1-26.

Chiwome, E. (1990). “The Role of Oral Traditions in the War of National Liberation in Zimbabwe: Preliminary Observations.” *Journal of Folklore Research*. Juz. 27: 241-247.

Ciulla, J.B. (2005). “Introduction”. Katika J.B. Ciulla, T.L. Price, S.E. Murphy (Wah.), *The Quest for Moral Leaders: Essays on Leadership Ethics, New Horizons in Leadership Studies*. Northampton, MA: Edward Elgar, Cheltenham. Kur. 1–9.

Davis, S. (2012). “Liveness, Mediation and Immediacy – Innovative Technology Use in Process and Performance”. *Research in Drama Education: The Journal of Applied Theatre and Performance*, 17: 501–516. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/13569783.2012.727623. Ilisomwa tarehe 20 Februari 2022.

Fetzer, A. (2020). ““And I Quote”: Forms and Functions of Quotations in Prime Minister’s Questions.” *Journal of Pragmatics*. Juz. 157: 89-100. Inapatikana katika https://doi.org/10.1016/j.pragma.2019.05.004. Ilisomwa 13 Machi 2022.

Fetzer, A. na Weiss, D. (2020). “Doing Things with Quotes: Introduction.” *Journal of Pragmatics*. Juz. 157: 84-88. Inapatikana katika https://doi.org/10.1016/j.pragma.2020.01.001

Gross, J. (2001). *Speaking in Other Voices: An Ethnography of Walloon Puppet Theaters*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Hadley, B. (2017). *Theatre, Social Media, and Meaning Making*. Cham: Springer International Publishing: Palgrave Macmillan.

Halliday, M.A.K. na Hasan, R. (2009). *Cohesion in English*. English Language Series. London: Longman.

Hanks, W.F. (1989). “Text and Textuality.” *Annual Review of Anthropology*. Juz. 18: 95-127. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/2155887. Ilisomwa 05 Februari 2022.

Holquist, M. (1981). “Introduction”. Katika M. Holquist (Mh.), *The Dialogic Imagination: Four Essays.* Mfasiri M. Holquist. Austin: University of Texas Press. Kur. xv–xxxiv.

Ibhawoh, B. na Dibua, J.I. (2003). “Deconstructing Ujamaa: The Legacy of Julius Nyerere in the Quest for Social and Economic Development in Africa.” *African Journal of Political Science*. Juz. 8: 59-83.

Jabir, S., Murunga, J. (Watayarishaji) (2015). *Mkasi with Mh. Tundu Lissu - Extended Version*. Inapatikana katika https://www.youtube.com /watch?v=1m8IRbqFnb0. Ilitazamwa 20 Machi 2022.

Jackson, R.H. na Rosberg, C.G. (1982). *Personal Rule in Black Africa: Prince, Autocrat, Prophet, Tyrant*. Berkeley, Calif: University of California Press.

Kibiriti, R. (2016). "Dk. Magufuli, Wembe ni Ule Ule, Usigeuke Jiwe". *Nipashe*. Tarehe 20 Julai 2016. Inapatikana katika https://www.ippmedia.com/sw/makala/dk-magufuli-wembe-ni-ule-ule-usigeuke-jiwe.

Lotman, Y.M. (1988). "Text within a Text." *Soviet Psychology*. Juz. 26 (3): 32–51. Inapatikana katika https://doi.org/10.2753/RPO1061-0405260332.

Mnenuka, A. (2019). "Public Policy Challenges in Tanzania as Portrayed in Swahili Written Literature." *Kiswahili*. Juz. 19: 156–73.

__________ (2019). "Utendajipepe wa Fasihi Simulizi: Haja ya kuwa na Tawi Jipya." *Eastern African Literary and Cultural Studies*. Juz. 3-4: 170–190. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/23277408.2019.1685583

__________ (2021). "Fluidity and Fixity of Performer, Audience and Performing Space." *UMMA*. Juz. 8: 35–51.

Nassor, E. (2018). Mziki wa Dansi Zilipendwa-Wahujumu na Walanguzi. Unapatikana katika https://www.youtube.com/watch?v=erJpQwg8d8Q. Ulitazamwa tarehe 15 Juni 2022.

Nkrumah, K. (2009). *Consciencism: Philosophy and Ideology for De-Colonization*. New York: Monthly Review Press.

Nuxoll, C. (2014). "Borrowed Tunes. Commando and Morale Booster Songs of RUF Fighters in the Sierra Leone War." *Transposition: Musique et Sciences Sociales*. Juz. 4. Inapatikana katika https://journals.openedition.org /transposition/598?lang=en . Ilisomwa tarehe 30 Machi 2022.

Nyerere, J.K. (1966). "President's Inaugural Address." In *Freedom and Unity/Uhuru na Umoja*. Nairobi: Oxford University Press. Kur. 176-187.

Orr, M. (2011). "Intertextuality". Katika M. Ryan, G. Castle, R. Eaglestone na M.K. Booker (Wah.), *The Encyclopedia of Literary and Cultural Theory*. Malden, MA: Wiley-Blackwell. Kur. 641-45.

Pechey, G. (2007). *Mikhail Bakhtin: The Word in the World. Critics of the Twentieth Century*. London; New York: Routledge.

Peirce, C.S. na Hoopes, J. (1991). *Peirce on Signs: Writings on Semiotic*. Chapel Hill: University of North Carolina Press.

Penfield, J. (1983). *Communicating with Quotes: The Igbo Case.* Contributions in Intercultural and Comparative Studies. Westport, Conn: Greenwood Press.

Radloff, B. (1993). "Text". Katika I.R. Makaryk (Mh.), *Encyclopedia of Contemporary Literary Theory: Approaches, Scholars, Terms*. Toronto: University of Toronto Press.

Rettová, A. (2010). "Philosophy in Utenzi Metre: Expression of Ideas and Values in Postindependence Swahili Historiographic Poetry." *Swahili Forum*. Juz. 17: 34-57.

Rolston, B. (2010). “Trying to Reach the Future through the Past: Murals and Memory in Northern Ireland.” *Crime, Media, Culture*. Juz. 6: 285-307. https://doi.org/10.1177/1741659010382335

Scholarios, D., Hesselgreaves, H. na Pratt, R. (2017). “Unpredictable Working Time, Well-being and Health in the Police Service.” *The International Journal of Human Resource Management*. Juz. 28(16):2275-2298. https://doi.org/10.1080/09585192.2017.1314314

Silverstein, M. na Urban, G. (1996). “The Natural History of Discourse.” Katika M. Silverstein na G. Urban (Wah.), *Natural Histories of Discourse*. Chicago: University of Chicago Press. Kur. 1-17.

Sulemana, I., Iddrisu, A.M. na Kyoore, J.E. (2017). “A Micro-Level Study of the Relationship between Experienced Corruption and Subjective Wellbeing in Africa.” *The Journal of Development Studies*. Juz. 53: 138-155. https://doi.org/10.1080/00220388.2016.1187721. Ilisomwa tarehe 15 Aprili 2022.

Urban, G. (1996). Entextualization, Replication, and Power. Katika M. Silverstein na G. Urban (Wah.), *Natural Histories of Discourse*. Chicago: University of Chicago Press. Kur. 21-44.

Vaz da Silva, F. (2012). “Tradition Without End”. Katika R. Bendix na G. Hasan-Rokem (Wah.) *A Companion to Folklore*. Blackwell Companions to Anthropology. Malden, MA: Wiley-Blackwell. Kur. 40-54.

Wales, K. (2011). *A Dictionary of Stylistics* (Toleo la 3). Harlow Munich: Longman.

Wilson Jr., J.A. (2006). “Political Songs, Collective Memories, and Kikuyu Indi Schools.” *History in Africa*. Juz. 33: 363-388.

Witte, H.D. (1999). “Job Insecurity and Psychological Well-being: Review of the Literature and Exploration of Some Unresolved Issues.” *European Journal of Work and Organizational Psychology*. Juz. 8: 155-177.

Wunderer, M. (1999). “Presence in Front of the Fourth Wall of Cyberspace”. Katika S.A. Schrum, (Mh.), *Theatre in Cyberspace : Issues of Teaching, Acting and Directing*. New York: P. Lang. Kur. 203-220.

Yankah, K. (2012). *The Proverb in the Context of Akan Rhetoric*. New York: Diasporic African Press.

**Viambatisho**

Eddie Nassor (2014) “Wahujumu na Walanguzi”. *Asilia Jazz Band.* Inapatikana katika https://www.youtube.com/watch?v=erJpQwg8d8Q

Jaston Binala (2018) “Nyerere na Hadithi ya Posa”. Inapatikana katika https://www.youtube.com/watch?v=aVvI2i3_ZC8&t=11s